ISSN 1866-5866 JANUARI-MACHI 2026

THE VOICE OF
Haki

# MAFANIKO THBUB NI JUHUDI ZA WATUMISHI, WANANCHI NA VIONGOZI WA UMMA:



**Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB), imepongezwa kwa kazi kubwa inazozifanya katika kulinda na kuhifadhi haki za binadamu na kusimamia misingi ya utawala bora nchini.**

Waziri wa nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Mhe. Haroun Ali Suleiman ametoa pongezi hizo alipowasilisha Ripoti ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ya mwaka wa fedha 2023/2024 katika Ukumbi wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Februari 25, 2026.

Mhe.Haroun ameeleza kuwa mafanikio makubwa yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu ya Tume yametokana na juhudi kubwa za watumishi, wananchi na viongozi wa umma chini ya uongozi imara wa Serikali zote, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ya Mapinduzi ya Zanzibar

Aidha, Mhe. Haroun amesema kuwa ripoti hiyo imeeleza hali ya haki za binadamu kwa maeneo ya Tanzania Bara na Zanzibar, ambapo imeonesha maeneo matatu muhimu yaliyoainishwa ndani yake ikiwemo eneo la Ulinzi wa Haki za Binadamu na Misingi ya Utawala Bora.

Kwa mwaka wa fedha 2023/24, ripoti inaonyesha THBUB kwa upande wa Zanzibar ilipokea malalamiko 103 yaliyohusu uvunjifu wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora na kufanyiwa kazi.

Ripoti hiyo pia imeeleza kuwa THBUB ilifanya uangalizi wa zoezi la uandikishaji wa wapiga kura katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa maeneo ya Kaskazini B na Magharibi B kwa Unguja na Wilaya za Chakechake, Micheweni na Mkoani Pemba.

Akieleza tathmini ya hali halisi ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora kwa mujibu wa katiba ya Zanzibar ya waka 1984, Waziri Haroun alieleza mafanikio ya THBUB katika kusimamia haki zikiwemo haki ya kuishi, haki ya usawa mbele ya sheria, haki ya kufanya kazi na kupata ujira, haki ya kujieleza, haki ya kushiriki katika shughuli za umma, kupata elimu, pamoja na haki za makundi maalumu katika jamii.

Mhe. Haroun alibainisha kuwa kwa ujumla Ripoti ya THBUB ya 2023-2024 imeakisi taswira halisi ya utekelezaji wa majukumu ya THBUB ya kuhamasisha, kulinda na kuhifadhi haki za binadamu na misingi ya utawala bora, Zanzibar.

# UTANGULIZI



Bw. Patience Ntwina
Katibu Mtendaji-THBUB

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ni Taasisi ya Kitaifa ya Haki za Binadamu yenya jukumu la kuhamasisha nchini ulinzi na hifadhi ya haki za binadamu na wajibu kwa jamii kwa mujibu wa katiba na sheria za nchi.

THBUB imeanzishwa chini ya inbara ya 129(1) ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Pamoja na jukumu hilo, THBUB pia hushughulikia malalamiko ya wananchi yanayohusu uvunjifu wa haki za binadamu, kufanya utafiti na ufuatiliaji wa masuala ya haki za binadamu na utawala bora sambamba na kutoa elimu.

Uanzishwaji wa jarida la Voice ya Haki Kumelenga kutoa taarifa ya kazi mbalimbali zinazofanywa na THBUB ili kuwezesha jamii kuwa na uelewa kuhusu majukumu ya Tume na namna yanavyotekelezwa katika kulinda na kukuza haki za binadamu na misingi ya utawala bora.

Hivyo, nichukue fursa hii kuwakaribisha kusoma jarida la robo ya tatu kwa mwaka 2025/2026 ili kuweza kuifahamu THBUB na majukumu yake

KAMATI YA UHARIRI
**Mwenyekiti:**
**Monica Mnanka**
Mhariri:
**Zawadi Msalla**
**Mhariri Msaidizi:**
**Nuru Mfaume**
Wajumbe:
**Mwashamba Juma**
**Tumaini Obel**
**Farida Ruben**
USANIFU
**Baraka Mgulu**
MAWASILIANO
**Makole,**
**Jengo PSSSF**
**S.L.P 1049 DODOMA,**
**Tanzania**
**Simu: +255 738 279744**
**Barua Pepe:**
**www.chragg.go.tz**

# YALIYOMO

MAFANIKO THBUB NI JUHUDI ZA WATUMISHI, WANANCHI NA VIONGOZI WA UMMA: WAZIRI HAROUN. UK 1.

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA YASHINDA KESI DHIDI YA TLS. UK 3.

WANAWAKE THBUB WASHIRIKI MAADHIMISHO YA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI. UK 4.

WATUMISHI THBUB WATAKIWA KUTAMBUA HAKI NA WAJIBU WAO. UK 5.

ZIARA YA IDARA YA UTAWALA NA RASILIMALI WATU YAIMARISHA UWAJIBIKAJI NA MAADILI KATIKA OFISI ZA MATAWI YA THBUB. UK 6.

THBUB YAHIMIZA WANAWAKE WAVUVI KUZIFAHAMU NA KUZILINDA HAKI ZAO. UK 7.

THBUB UNGUJA, PEMBA KUIMARISHA USHIRIKIANO. UK 8.

HABARI PICHA . UK 9,10,11,12 & 13.

# TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA YASHINDA KESI DHIDI YA TLS



Mahakama Kuu ya Tanzania kanda ya Dar es Salaam imeitupilia mbali shauri la kikatiba lililofunguliwa na Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) dhidi ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB), Inspekta Jenerali wa Polisi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Katika shauri hilo, TLS ilidai kuwa THBUB ilishidwa kutekeleza jukumu la kulinda haki za binadamu katika kipindi cha amri ya kutotoka nje iliyotolewa na Inspekta Jenerali wa Polisi tarehe 29 Oktoba, 2025 na hivyo kuitaka Mahakama kutamka kuwa amri hiyo ilikiuka haki za binadamu.

TLS ilidai kuwa haki za msingi za binadamu, ikiwemo haki ya uhuru wa mtu binafsi, uhuru wa kutembea pamoja na haki ya kuishi zilikiukwa, na kwamba THBUB haikutekeleza ipasavyo wajibu wake wa kulinda na kutetea haki hizo wakati wa utekelezaji wa amri ya kutotoka nje.

Aidha, TLS iliomba Mahakama kuunda Tume huru ya uchunguzi yenye wajumbe saba kutoka Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, Chama cha Mawakili Tanganyika, Chama cha Madaktari, Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa na Jumuiya ya Madola ili kuchunguza hatua zilizochukuliwa na Inspekta Jenerali wa Polisi kuhusu utekelezaji wa amri hiyo.

Katika usikilizwaji wa shauri hilo, THBUB iliwakilishwa na jopo la mawakili likiongozwa na Wakili Msomi Bi. Ellen Rwijage ambaye ni Mkurugenzi wa Huduma za Kisheria kwa kushirikiana na wakili msomi Rosemary Shio, wakili msomi Pontian Kitorobondo, wakili msomi Majid Kangile na wakili msomi Joshua Matiku wote kutoka THBUB na Mawakili Wasomi kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Upande wa THBUB uliieleza Mahakama kuwa haina mamlaka ya kuunda Tume ya Uchunguzi kama ilivyokuwa ikiombwa na TLS, kwani kwa mujibu wa kifungu cha 3(1) cha Sheria ya Tume ya Uchunguzi mamlaka hayo yapo kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pekee.

Baada ya kusikiliza hoja za pande zote, Mahakama ilikubaliana na hoja za THBUB kwamba Mahakama Kuu haina mamlaka ya kuunda Tume ya Uchunguzi kama ilivyokuwa ikiombwa na TLS, kwani mamlaka hayo kisheria yapo kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pekee.

Aidha, Mahakama ilibainisha kuwa hati ya kiapo iliyowasilishwa kuunga mkono madai hayo ilikuwa na kasoro, ikiwemo kuwepo kwa tarehe zisizolingana kuhusu utolewaji wa amri ya kutotoka nje.

Kutokana na kasoro hizo za kisheria, Mahakama iliamua kutupilia mbali shauri hilo kwa kuwa halikuwa na uhalali wa kisheria wa kuendelea kusikilizwa, huku kila upande ukibeba gharama za kesi.

Uamuzi huo uliotolewa Machi 11, 2026 na Waheshimiwa Jaji Banzi, Jaji Mtulya na Jaji Mnyukwa unaonesha umuhimu wa kufuata taratibu sahihi za kisheria katika kuwasilisha mashauri mahakamani.

# WANAWAKE THBUB WASHIRIKI MAADHIMISHO YA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI



Watumishi wanawake wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB), wameungana na wanawake wenzao kutoka taasisi za Serikali na binafsi katika mikoa minne kushiriki maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika tarehe 8 Machi 2026 katika maeneo mbalimbali nchini.

Ushiriki katika madhimisho hayo umefanyika katika mikoa ya Mtwara katika viwanja vya Saba-Saba, Dar es Salaam katika viwanja vya Barafu Ubungo, Mwanza katika viwanja vya Nane Nane Kisesa, huku kwa upande wa Dodoma yamefanyika katika viwanja vya Shule ya Mbande wilayani Kongwa, ambapo mgeni rasmi katika maadhimisho ya Dodoma alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mheshimiwa Rosemary Senyamule.

Maadhimisho ya mwaka huu yamefanyika chini ya kauli mbiu isemayo: “Haki kwa wanawake na wasichana ni msingi wa maendeleo jumuishi kufikia Dira ya 2050.” Kauli mbiu hiyo inalenga kuhamasisha jamii kutambua umuhimu wa kuhakikisha wanawake na wasichana wanapata haki na fursa sawa katika nyanja mbalimbali ikiwemo elimu, uchumi, uongozi na ushiriki katika maamuzi ya maendeleo.

Akizungumza katika maadhimisho hayo Jijini Dodoma, Mheshimiwa Senyamule alisisitiza kuwa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuwawezesha wanawake kiuchumi na kijamii ili waweze kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya nchi.






Aidha, amesisitiza umuhimu wa kulinda na kutetea haki za wanawake na wasichana, ameeleza kuwa jamii ina wajibu wa kuhakikisha vitendo vya ukatili wa kijinsia, ubaguzi na unyanyasaji vinatokomezwa ili kuweka mazingira salama na yenye usawa kwa wote.

Kwa upande wa THBUB, ushiriki wa watumishi wanawake wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora katika maadhimisho hayo ni sehemu ya jitihada za taasisi hiyo kuendelea kuhamasisha ulinzi na ukuzaji wa haki za binadamu, hususan haki za wanawake na wasichana. Kupitia majukumu yake ya kikatiba, Tume inaendelea kutoa elimu kwa umma, kupokea na kushughulikia malalamiko ya ukiukwaji wa haki za binadamu pamoja na kushauri Serikali na wadau mbalimbali kuhusu namna bora ya kuimarisha utawala bora na usawa katika jamii.

Kupitia maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, jamii imekumbushwa kuwa kulinda na kuheshimu haki za wanawake na wasichana si wajibu wa wanawake pekee bali ni jukumu la jamii nzima, hatua ambayo ni muhimu katika kujenga taifa lenye usawa, haki na maendeleo jumuishi



# WATUMISHI THBUB WATAKIWA KUTAMBUA HAKI NA WAJIBU WAO

Watumishi wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora wametakiwa kutambua haki, wajibu wao pamoja na kuzingatia maadili ili kuleta utendaji wenye tija, staha na heshima mahala pa kazi.

Hayo, amesema Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Bw. Patience Ntwina wakati akifungua Mkutano wa 24 wa Baraza la Wafanyakazi uliofanyika Februari 11, 2026 ukumbi wa NALA Hoteli, Jijini Dodoma.



Bw. Ntwina amesema kuwa Baraza la Wafanyakazi ni Chombo muhimu kinacho wawezesha watumishi kupitia wawakilishi wao kujadili masuala yanayohusu maslahi yao na mahusiano kati yao na mwajiri.

“Mabaraza haya yameundwa kisheria kama vyombo vya ushauri mahala pa kazi kwa lengo la kuongeza tija, kuimarisha mshikamano kati ya watumishi na mwajiri sambamba na kutekeleza wajibu ili kufikia malengo.

Bw. Ntwina ameeleza kuwa mkutano huo pia unalenga kujadili utekezaji wa majukumu ya THBUB kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na kujadili mapendekezo ya mpango wa bajeti ya mafungu madogo kwa mwaka 2026/2027



“Ni mategemeo yangu kuwa wajumbe mtajadili kwa makini na kutoa maoni yenye kuleta tija katika utekelezaji wa majukumu yetu na kufikia malengo ya taasisi na tuhakikishe majadiliano yanaongozwa na hekima, busara, uwazi na maelewano yatakayotatua changamoto zetu ” amesema Bw. Ntwina.

Aidha, Bw. Ntwina ametoa wito kwa wajumbe hao kujadili kwa kina malengo na mipango ya THBUB, ikiwemo maslahi ya watumishi, njia za kuboresha utendaji kazi ili kuongeza tija na utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

# ZIARA YA IDARA YA UTAWALA NA RASILIMALI WATU YAIMARISHA UWAJIBIKAJI NA MAADILI KATIKA OFISI ZA MATAWI YA THBUB

Katika jitihada za kuimarisha utendaji kazi na kuongeza ufanisi wa utoaji huduma kwa wananchi, Viongozi wa Idara ya Utawala na Rasilimali Watu Katika Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB), wamefanya ziara katika ofisi za matawi ya Dar es Salaam, Mwanza na Zanzibar kwa lengo la kufuatilia utendaji kazi, kusisitiza maadili ya utumishi wa umma na kuhamasisha uwajibikaji miongoni mwa watumishi.

Ziara hiyo imeongozwa na Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu, Bw. Jackson Nyamwihula kwa kushirikiana na Mkurugenzi Msaidizi wa Rasilimali Watu, Bw. Johnston Mwakalitolo ambao walikutana na watumishi katika ofisi za matawi na kutoa maelekezo mbalimbali yanayolenga kuboresha utendaji kazi wa taasisi.

Akizungumza kwa nyakati tofauti za ziara hiyo, Bw. Nyamwihula alisisitiza umuhimu wa watumishi kutekeleza majukumu yao kwa weledi, kuzingatia miongozo na taratibu zilizowekwa pamoja na kudumisha nidhamu ya kazi ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora na kwa wakati.

Alieleza kuwa uwajibikaji, uadilifu na nidhamu ni misingi muhimu ya utumishi wa umma, huku akiwataka watumishi kujiepusha na vitendo vya rushwa na kuzingatia maadili ya kazi katika kuwahudumia wananchi kwa heshima na haki.

Kwa upande wake, Bw. Mwakalitolo alibainisha kuwa utumishi wa umma unahitaji watumishi wenye uaminifu, bidii na uwajibikaji, akisisitiza matumizi sahihi ya rasilimali za umma na umuhimu wa kujenga imani ya wananchi kwa THBUB



"Mtumishi wa umma anatakiwa kufanya kazi kwa haki, kuheshimu wananchi na kutumia rasilimali za umma kwa uangalifu ili kuimarisha ufanisi wa taasisi na kuleta matokeo chanya kwa jamii," alisisitiza.

Katika ziara hiyo, Mwenyekiti wa TUGHE tawi la THBUB, Bw. Pontian Kitorobombo, alitoa elimu kwa watumishi kuhusu umuhimu wa kujiunga na chama hicho, akieleza kuwa uanachama unaleta manufaa mbalimbali ikiwemo ulinzi wa maslahi ya mtumishi na kushiriki katika mifuko ya kijamii kama mfuko wa kufarijiana.

Watumishi katika matawi ya Dar es Salaam, Mwanza na Zanzibar waliwashukuru viongozi hao kwa ziara hiyo, wakieleza kuwa imewapa hamasa mpya na mwelekeo bora katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku. Waliahidi kuendelea kuzingatia maadili ya utumishi wa umma kwa kufanya kazi kwa uaminifu, uwajibikaji na bidii.

Kwa ujumla, ziara hiyo imekuwa chachu ya kuimarisha mshikamano, kuongeza ufanisi wa kazi na kuendelea kuboresha utoaji wa huduma bora kwa wananchi, sambamba na kuendeleza misingi ya haki, usawa na utawala bora nchini.





# THBUB YAHIMIZA WANAWAKE WAVUVI KUZIFAHAMU NA KUZILINDA HAKI ZAO




Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB), Bw. Patience Ntwina, amewahimiza wanawake wavuvi nchini kuwa na uelewa na kudai haki zao za msingi ili kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya sekta ya uvuvi.

Bw. Ntwina ametoa wito huo wakati akifungua mafunzo ya siku mbili kwa viongozi wa Mtandao wa Wanawake Wanaojihusisha na Shughuli za Uvuvi Tanzania (TAWFA), yaliyoandaliwa na THBUB kwa kushirikiana na Taasisi ya Haki za Binadamu ya Denmark (DIHR), yaliyofanyika Mjini Morogoro Februari 5 hadi 6, 2026.

Akielezea lengo la mafunzo hayo, Bw. Patience Ntwina, amesema kuwa lengo kuu la mafunzo hayo ni kuwawezesha wanawake wavuvi kuelewa haki zao za msingi, kuzidai pale zinapokiukwa na kuwa mabalozi wa utetezi wa haki za binadamu katika jamii zao.

"THBUB ina wajibu wa kuhakikisha haki za binadamu zinakuzwa, zinalindwa na kuhifadhiwa kwa usawa katika nyanja zote za kijamii, kiuchumi na kiutamaduni, hususan kwa makundi yaliyo katika mazingira hatarishi kama wanawake wavuvi wadogo," amesema Bw. Ntwina.

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Uvuvi, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Bi. Margrethe Dominic, Akizungumza katika mafunzo hayo kwa niaba ya Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Uvuvi, Wizara ya Mifugo na Uvuvi amesema kuwa sekta ya uvuvi nchini Tanzania inategemea zaidi wavuvi wadogo wanaofikia asilimia 90, huku wanawake wakichangia kwa kiwango kikubwa katika kuongeza thamani ya mazao ya uvuvi.

Aidha, Mwenyekiti wa TAWFA Taifa, Bi. Beatrice Mmbaga, amesema kwa niaba ya washiriki wa mafunzo hayo wanaishukuru THBUB kwa kuandaa mafunzo hayo na kwamba kupitia THBUB washiriki wamepata elimu kuhusu misingi ya haki za binadamu, mbinu za utetezi, usimamizi shirikishi wa rasilimali za maji, pamoja na namna ya kuwasilisha malalamiko ya uvunjifu wa haki zao katika mamlaka husika ikiwemo THBUB.

Mafunzo hayo yaliwakutanisha viongozi wa TAWFA kutoka maeneo mbalimbali ya uvuvi ikiwemo bahari, Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika, pamoja na vyanzo vidogo vya maji. Pia yalihusisha wawakilishi kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) pamoja na watumishi wa THBUB.

# THBUB UNGUJA, PEMBA KUIMARISHA USHIRIKIANO



Watumishi wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) ofisi ya Zanzibar walifika katika kijiji cha Dunga Kiembeni Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja Februari 17, 2026 na kutoa elimu ya haki za binadamu na utawala bora.

Akiwasilisha mada kuhusu majukumu ya THBUB kwa wakazi wa kijiji hicho wakati wa mkutano wa pamoja baina ya THBUB na wakazi hao, Afisa Sheria wa THBUB Bw. Wilfred Msagati amewahimiza kuwasilisha THBUB malalamiko juu ya uvunjifu wa haki zao na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora.

Msagati ametaja baadhi ya majukumu ya THBIUB kuwa ni pamoja na kuhamasisha nchini hifadhi ya haki za binadamu na wajibu kwa jamii , kueneza elimu ya haki za binadamu na utawala bora, kufanya utafiti, kupokea malalamiko, kufanya uchunguzi, kutembelea na kukagua maeneo wanamozuiliwa watu kwa mujibu wa Sheria

Naye, Afisa Uchunguzi wa THBUB, Bw. Abdullatif Ali Sheha wakati akiwasilisha mada ya "Haki za Binadamu na Misingi ya Utawala Bora" kwa wananchi wa kijiji hicho, amesema lengo la mkutano huo ni kuwajengea uelewa wananchi hao ili watambue haki zao na wajibu wao katika kulinda haki za binadamu na misingi ya utawala bora.

Kwa upande wa wanchi hao, wameishukuru na kuipongeza THBUB kwa jitihada zao za kuwafikia wananchi wa vijijini kwa kutoa elimu pamoja na kusikiliza changamoto zinazowakabili.



# HABARI PICHA



Aliyekuwa Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Mhe. Mathew P. M Mwaimu (Jaji (Mst.) wa tatu kushoto waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na waheshimiwa Makamishna waliomaliza muda wao na watumishi wa tume hiyo wakati wa hafla ya kuwaaga wanatume hao waliostaafu utumishi wa umma iliyofanyika katika eneo la Peace Yard, Jijini Dodoma Januari 15, 2026.



Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Bw. Patience Ntwina (Kushoto) akikabidhi Zawadi kwa aliyekuwa Mwenyekiti wa THBUB Mhe. Mathew P. M Mwaimu (Jaji Mst) katika hafla fupi ya kuwaaga Makamishna iliyofanyika katika eneo la Peace Yard Jijini Dodoma Januari 15, 2026

# HABARI PICHA



Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Bw. Patience Ntwina akizungumza na wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wakati wa kikao cha 24 kilichofanyika Ukumbi wa NALA Hoteli, Jijini Dodoma Februari 11, 2026.



Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora , Bw. Patience Ntwina (katikati waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi, baadhi ya Wakurugenzi wa Idara na Wakuu wa Vitengo mara baada ya kumalizika kwa kikao cha 24 cha baraza hilo kilichofanyika katika Ukumbi wa Nala Hoteli, Jijini Dodoma Februari 11, 2026.

# HABARI PICHA




Naibu Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za binadamu na Utawala Bora Zanzibar, Bw. Juma Msafiri Karibona akizungumza katika kikao cha pamoja baina ya watumishi wa ofisi hiyo Unguja na Ofisi ya Pemba kupitia njia ya mtandao (zoom meeting). Mkutano huoulifanyika ofisi za Tume zilizopo Mombasa, Wilaya ya Magharibi B Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja, Machi 4, 2026.



Afisa Uchunguzi wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, THBUB ofisi ya Zanzibar, Bw. Abdullatif Ali Sheha (kushoto aliyesimama) akiwasilisha mada ya "Haki za Binadamu na Misingi ya Utawala Bora" kwa wananchi wa kijiji cha Dunga Kiembaeni, Wilaya ya Kati Mkoa wa Kusini Unguja, Februari 17, 2026.

# HABARI PICHA




**Baadhi ya Watumishi Wanawake wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Makao Makuu Dodoma wakiwa katika maandamano ya kuadhimisha Siku ya Wanawake yaliyofanyika Viwanja vya Shule ya Msingi Mbande Wilaya ya Kongwa, Jijini Dodoma Machi 8, 2026**



**Baadhi ya Watumishi Wanawake wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Tawi la Mwanza wakiwa wameungana na wanawake wengine kutoka Taasisi binafsi na Serikali wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake yaliyofanyika Viwanja vya Nanenane Kisesa Machi 8, 2026**

# HABARI PICHA



Katibu Mtendaji Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, (THBUB) Bw. Patience Ntwina akifungua mafunzo maalum kwa viongozi wa Mtandao wa Wanawake Wanaojihusisha na Shughuli za Uvuvi Tanzania (TAWFA) yaliyofanyika Mjini Morogoro Februari 5, 2026




Katibu Mtendaji Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, (THBUB) Bw. Patience Ntwina (Katikati) akiwa katika picha ya pamoja na viongozi wa Mtandao wa Wanawake Wanaojihusisha na Shughuli za Uvuvi Tanzania (TAWFA), wakati wa kikao kilichofanyika Mjini Morogoro Februari 5, 2026.

# HABARI PICHA




**Mkurugenzi Msaidizi wa Rasilimali Watu wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, (THBUB) Bw. Johnston Mwakalitolo akizungumza na watumishi wa THBUB tawi la Zanzibar Machi 5, 2026.**

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

TANZANIA
COMMISSION FOR HUMAN RIGHTS
AND GOOD GOVERNANCE